

# **ATLASI YA LUGHA ZA TANZANIA**

**MRADI WA LUGHA ZA TANZANIA**



**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**2009**

Mradi wa Lugha za Tanzania  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
S.L.P. 35040  
Dar es Salaam

Tovuti: <http://www.lot.udsm.ac.tz>

© Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 2009

Ramani zimesanifiwa na kuchapwa na InfoBridge Consultants Ltd

ISBN 978 9987 691 26 5

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu ya kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya Mradi wa Lugha za Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## YALIYOMO

Shukurani	iv
Utangulizi wa Jumla	v
Lugha za Tanzania	1
Orodha ya Lugha za Tanzania kwa Ukubwa	2
Orodha ya Lugha za Tanzania kwa Alfabeti	3
Lugha Kuu Ishirini katika Ramani	4
Mkoa wa Arusha	6
Mkoa wa Dodoma	12
Mkoa wa Iringa	18
Mkoa wa Kagera	24
Mkoa wa Kigoma	30
Mkoa wa Kilimanjaro	36
Mkoa wa Lindi	42
Mkoa wa Manyara	48
Mkoa wa Mara	54
Mkoa wa Mbeya	60
Mkoa wa Morogoro	66
Mkoa wa Mtwara	72
Mkoa wa Mwanza	78
Mkoa wa Pwani	84
Mkoa wa Rukwa	90
Mkoa wa Ruvuma	96
Mkoa wa Shinyanga	102
Mkoa wa Singida	108
Mkoa wa Tabora	114
Mkoa wa Tanga	120
Faharasa ya Kata na Wilaya	126
Faharasa ya Lugha	130

## SHUKURANI

Kazi ya kuandaa atlas hii imechukua muda mrefu na imechangiwa na watu wengi kwa nyakati tofauti. Ni vigumu kuwataja watu wote waliotoa mchango wao katika kazi hii ngumu. Hata hivyo hatuna budi kuwatambulisha baadhi ya wahusika wakuu.

### 1. Waratibu wa Mradi wa Lugha za Tanzania

Josephat Rugemalira  
Henry Muzale

### 2. Kamati ya Usimamizi wa Mradi

William Rugumamu  
Chachage S. Chachage  
David Massamba  
Kulikoyela Kahigi  
Casmir Rubagumya  
Michael Kadeghe  
Deoscorous Ndoloi  
Henry Muzale  
Josephat Rugemalira

### 3. Kikosi cha Watafiti

Josephat Rugemalira  
Henry Muzale  
David Massamba  
Casmir Rubagumya  
Yunus Rubanza  
Abel Mreta  
Selemani Sewangi  
James Mdee  
Kulikoyela Kahigi  
George Mrikaria  
Josephat Maghway  
John Kiango  
Zakaria Mochiwa  
Norbert Mtavangu  
Nikuigize Shartiely  
Rahma Muhdhar  
Rose Upor  
Martha Qorro  
Azaveli Lwaitama  
Yared Kihore  
Gastor Mapunda

### 4. Jopo la Wahariri

Josephat Rugemalira  
Henry Muzale  
David Massamba  
Kulikoyela Kahigi  
Azaveli Lwaitama  
Abel Mreta  
Yared Kihore

### 5. Kitengo cha Kuhakiki Takwimu

Henry Muzale  
Julius John  
Kelvin Mathayo  
Yunus Ng'umbi  
Nicholaus Asheli  
Davis Nyanda  
Edwin Msambwa

### 6. Tunatoa shukurani kwa mtafiti mshiriki

Prof. Karsten Legere, wa Chuo Kikuu cha Gotebogi, Uswidi.

### 7. Wataalamu wa Usanifu na Uchoraji Ramani

InfoBridge Consultants Ltd

### 8. Tunatoa shukurani za pekee kwa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uswidi (SIDA) kwa kufadhili shughuli za Mradi wa Lugha za Tanzania.

## UTANGULIZI WA JUMLA

Utangulizi huu una sehemu sita. Sehemu ya kwanza inahusu sera ya lugha na utafiti kuhusu lugha za asili, na mustakabali wake. Sehemu ya pili inahusu maandiko katika au kuhusu lugha za asili. Sehemu ya tatu inahusu uainishaji wa lugha za Tanzania kinasaba. Sehemu ya nne inazungumzia istilahi zilizotumika katika atlas hii. Sehemu ya tano inahusu maudhui ya atlas na mbinu za utafiti na utengenezaji wa ramani. Sehemu ya sita inatoa orodha ya machapisho ya Mradi wa Lugha za Tanzania.

### 1. LUGHA ZA ASILI NA MUSTAKABALI WAKE

#### Historia ya Mradi wa Lugha za Tanzania

Mradi wa Lugha za Tanzania ulizinduliwa mwaka 2001 katika Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nia ya Mradi wa Lugha za Tanzania ni kuzikuza lugha hizi kwa ajili ya matumizi ya jamii, na kuzihifadhi kwa ajili ya kumbukumbu ya vizazi vijavyo. Nia hii inawiana na malengo yaliyoainishwa katika *Sera ya Utamaduni* (Wizara ya Elimu na Utamaduni 1997:17–18) inayotamka haja ya:

- kutafiti, kuhifadhi, na kutafsiri lugha za jamii;
- kuandika kamusi na sarufi za lugha za jamii;
- kuchapisha maandiko mbalimbali katika lugha za jamii.

Hadi sasa mradi huu umekwishachapisha vitabu vipatavyo ishirini na vinne vya kamusi, sarufi na hadithi katika lugha mbalimbali za Tanzania (tazama sehemu ya sita). Pia makala mbalimbali zimechapishwa katika majarida na vitabu mbalimbali vya masuala ya isimu ya lugha. Atlas ya lugha za Tanzania ni chapisho linalochukua nafasi ya pekee katika mfululizo wa machapisho haya ya mradi. Licha ya machapisho, mradi huu pia umechangia kuelimisha wataalamu wa kutafiti miundo na isimujamii ya lugha za Tanzania. Vilevile, katika mikutano na semina mbalimbali, mradi umesaidia kuhamasisha jamii ya Watanzania izipatie lugha hizi fursa pana zaidi ya kutumika katika maisha ya kila siku.

#### Matumizi ya Lugha za Tanzania

Watanzania walio wengi, pamoja na kutumia Kiswahili kama lugha ya Taifa, vilevile wanatumia lugha zao za asili katika mawasiliano ya kila siku. Lugha hizi hutumiwa hasa katika maeneo ya vijijini. Kwa mfano, katika shughuli za uchumi, hasa kilimo, ufugaji na uvuvi, Watanzania wengi huwasiliana kwa kutumia lugha zao za asili. Kwa kuwa takribani asilimia 85 ya Watanzania wanaofanya kazi wanajishughulisha na kilimo, ni wazi kuwa lugha za asili zina umuhimu mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. Baadhi ya makabila, mathalani, huimba nyimbo kwa ajili ya kuhamasishana katika lugha za asili wakati wakiwa shambani. “Wimbo ukiimbwa pamoja huunganisha matendo na kuwafanya wafanyakazi wajisikie kufanya kazi kama kikundi na sio mtu mmoja. Mapigo ya wimbo huhamasisha ushirikiano. Kwa jinsi hii, watu hufanya kazi kwa nguvu, haraka na kwa kuifurahia” (Mtavangu, 2008:104).

Lugha za asili za Tanzania vilevile hubeba maarifa mengi ambayo wazungumzaji wa lugha hizo wanaweza kuyatumia kujitelea maendeleo. Maarifa hayo yanaweza kutumika katika shughuli za kiuchumi, tiba za asili, ibada, na kadhalika. Rubanza (2008) anatoa mfano wa lugha ya Kihaya huko mkoani Kagera kuonyesha jinsi lugha za asili zilivyosheheni maarifa. Mzungumzaji wa Kihaya anazipambanua aina zaidi ya 12 za ndizi. Hizi hutengwa katika makundi matatu: ndizi za kupika, za kutengeneza pombe na za kuliwa mbivu. Utafiti zaidi umebainisha kuwa lipo pia kundi la nne ambalo ni la ndizi za kuchoma. Katika ndizi za kupika kuna aina ambayo haifai kumlisha mtoto mdogo, kuna ambazo hazifai kumpa mtu mzima anayeumwa tumbo, na kadhalika. Vilevile, kila sehemu ya mgomba ina umuhimu wake na matumizi maalumu katika jamii ya Wahaya, kama vile mbolea, kamba za kufungia mizigo, ‘taulo’ ndogo ya kujipangusia mikono, na matumizi mengine mengi.

Maarifa katika lugha za asili pia hujikita katika methali, misemo, nyimbo na hadithi. Vyote hivi hubeba ujumbe mzito wa kuwafahamisha na kuwakanya wanajamii.

Kwa bahati mbaya, lugha nyingi za asili sasa hivi zinakabiliwa na kupungua kwa matumizi yake hata katika zile nyanja ambamo zilikuwa zinatumiwa. Kahigi (2008) ameanisha sababu mbalimbali zinazosababisha lugha hizi ziendelee kubanwa na Kiswahili, nazo ni pamoja na kukua kwa miji, ndoa mchanganyiko, na kutokutumika kwa lugha za asili katika mfumo wa elimu rasmi wala katika vyombo vya habari.

Hali ya kubanana kwa lugha mbalimbali huchochewa sana na mwingiliano wa jamii ambao huambatana na ukuaji wa miji. Miji hutoa mazingira muafaka ya kukuza lugha moja ya mawasiliano mapana kwa watu wazima. Miji pia hudhoofisha misingi ya kuendeleza lugha mbalimbali kwa kuwafanya watoto wengi wasijifunze lugha za wazazi wao. Hali hiyo inaonekana wazi zaidi katika ndoa zenye kuwahusu wasemaji wa lugha tofauti. Mara nyingi, katika ndoa za namna hiyo, watoto hawafundishwi lugha ya mzazi yeyote kwa kuwa lugha hiyo haizungumzwi nyumbani. Lakini hata kama wazazi wanazungumza lugha moja, hali ya miji huwalea watoto wenye kuzungumza lugha pana ya jamii na ambayo si lugha ya kwanza ya wazazi.

### Umuhimu wa Kukuza na Kuhifadhi Lugha za Tanzania

Ni ukweli usiohitaji mjadala kuwa binadamu katika jamii mbalimbali huhitaji lugha ili waweze kuwasiliana. Aidha, ni kwa njia ya mawasiliano binadamu wanaweza kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kidini, na kadhalika. Lugha vilevile ni utambulisho muhimu wa mtu binafsi na watu katika makundi yao kama vile kabila na taifa. Mshairi mmoja aliyeitwa Ignazio Buttita, akieleza umuhimu wa lugha, alisema:

Wafunge watu minyororo,  
wavue nguo,  
wazibe midomo yao,  
bado ni watu huru.

Wanyang'anye kazi zao,  
pasi zao za kusafiria,  
meza zao za chakula,  
bado ni matajiri.

Watu huwa fukara na watumwa,  
wanaponyang'anywa lugha yao,  
waliyoachiwa na wahenga wao,  
wanapotea milele  
(Tafsiri ya Ndagala 2008)

Kwa mtazamo wa mshairi huyu, harakati zozote za kumnyima mtu au kundi la watu fursa ya kutumia lugha yao ni kutowatendea haki. Ndiyo maana katika sehemu mbalimbali za dunia sasa hivi kuna mapambano ya watu kutaka lugha zao zipewe fursa ya kukua na kushamiri bila ya kuwekewa vikwazo vyovyote.

Ni lazima kuzikuza na kuzihifadhi lugha za Tanzania kama sehemu ya mkakati wa kujithamini kama binadamu na kuthamini utamaduni wetu. Kujithamini huko kutaiwezesha jamii yetu kujenga msingi wa kushiriki kikamilifu na kwa ushindani stahiki katika shughuli za ulimwengu wa utandawazi. Kujithamini kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii nzima kunajenga kujiamini katika kupambana na changamoto, kujifunza kutoka kwa watu na jamii nyingine, na kuchangia kuunda maarifa na utamaduni wa mwanadamu kwa jumla. Jamii isiyojithamini na kujiamini itakumbatia tu mambo yoyote yatokayo ughaibuni bila kujali kwamba kuna mchango uwezao kutoka nyumbani.

Kukuza lugha za jamii kutachangia kwa kiasi kikubwa kujenga miundo ya jamii iliyo mipana na wakilishi zaidi badala ya kutengeneza miundo yenye kushirikisha na kufaidisha matabaka fulani tu ya jamii. Na matumizi ya lugha za jamii zetu yatatuwezesha kusambaza maarifa ya jadi kutoka jamii moja kwenda jamii nyingine na kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

### Mwenendo wa Kubadilika kwa Lugha

Lugha zote za mwanadamu hubadilika siku hadi siku kiasi kwamba baada ya miongo na karne kadhaa wachunguzi makini wanaweza kuona tofauti kati ya lugha itumikayo sasa na ile ya awali. Lugha yaweza kugawanyika na wazungumzaji wakajikuta wanazungumza lugha mbili au tatu tofauti. Lugha pia inaweza kufa na vizazi vya baadaye vya jamii hiyo vikachukua lugha za majirani.

Mabadiliko ya lugha hayatokei kwa nasibu tu. Baadhi ya misongo inayoshinikiza mabadiliko katika lugha zetu katika zama hizi inaonekana kushika kasi waziwazi. Kwa kawaida, lugha ndogo inapopakana na lugha kubwa msongo wa lugha hii kubwa huipa changamoto lugha ndogo; wazungumzaji wa lugha ndogo huanza kuitumia ile lugha kubwa kama lugha yao ya pili na kadiri muda unavyopita, matumizi ya lugha kubwa huzidi kupanuka katika nyanja mbalimbali za jamii ya wazungumzaji wa ile lugha ndogo. Matumizi hayo huanza kuathiri msamiati na sarufi ya lugha ndogo kwa njia ya kukopa maneno na kuchanganya miundo kutoka lugha kubwa. Hatimaye watoto wasipopata fursa ya kufundishwa ile lugha ndogo, lugha hiyo hutoweka mara mzungumzaji wa mwisho wa lugha ile anapofariki.

Lugha zinazotoa msongo mkubwa kwa lugha nyingine huwa zina maslahi ya kiuchumi – zikizungumzwa na watu wengi zaidi, zenye kutoa fursa nyingi zaidi za kazi au biashara, na kumwezesha mzungumzaji kupanda ngazi zaidi katika mfumo wa jamii.

### Sera ya Lugha na Mustakabali wa Lugha za Asili

Sera ya lugha ya Tanzania inatambua lugha mbili tu, yaani Kiswahili na Kiingereza, kama lugha rasmi. Lugha za asili za Tanzania hazipewi fursa yoyote ya kutumika katika nyanja rasmi za elimu, utawala serikalini wala katika vyombo vya habari. Kumekuwa na matamko yanayoashiria kuwa msimamo wa serikali huko nyuma ni kutoruhusu lugha za asili kutumika katika vyombo vya habari. Tamko la kwanza lilichapishwa katika gazeti la *Nipashe* la tarehe 13 Agosti 1999:

....Serikali imesema haitasajili magazeti yanayochapishwa katika lugha za makabila, kwa kuwa itakuwa ni kupanda mbegu za ukabila nchini na kuchochea migawanyiko. [Ingawa] sheria ya magazeti ya mwaka 1976 haizungumzi chochote kuhusu usajili wa magazeti ya lugha za makabila [...] kama usajili wa aina hiyo utaruhusiwa itakuwa vigumu kwa serikali kufuatilia habari zinazochapishwa katika magazeti ya aina hiyo kwa kuwa lugha zitakazotumika hazitaeleweka kwa wengi. Haitakuwa rahisi kwa serikali kufuatilia mabaya ambayo yanaweza kuchapishwa na magazeti ya aina hiyo kwenye makabila yanayohusika.

Tamko la pili lilichapishwa kwenye gazeti la *Majira* la tarehe 30 Oktoba 2003 kuhusu matumizi ya lugha za asili kwenye redio:

....Serikali imepiga marufuku redio nchini kurusha matangazo kwa lugha za kienyeji na badala yake ni lugha za Kiswahili na Kiingereza tu ndizo zitatumika ... Msajili wa Tume ya Utangazaji ... alisema redio na televisheni yoyote itakayotangaza kwa lugha za kienyeji itapewa adhabu kutokana na kifungu cha sheria ya utangazaji ya mwaka 1993... Tume yake inatoa vibali vya kuanzisha redio za jamii na tayari imekwishatoa vibali kwa redio za jamii tatu zinazoongozwa na Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs), ambazo hata hivyo haziruhusiwi kuendesha matangazo kwa kilugha.

Hapa jambo linaloonekana wazi, hasa katika tamko la kwanza kuhusu magazeti, ni kwamba serikali inakataza matumizi ya lugha za asili katika vyombo vya habari kwa sababu mbili.

Sababu ya kwanza ni hofu ya “kupanda mbegu za ukabila”. Hapa serikali inasahau kuwa ukabila hauchochewi kwa watu kutumia lugha zao katika shughuli zao za kila siku, au kutumia lugha hizo kupeana taarifa na kuelimishana. Mara nyingi machafuko katika jamii huletwa na mfumo unaowakandamiza baadhi ya watu katika jamii, na mgawanyo wa rasilimali usio wa haki. Kama kutumia lugha moja katika taifa ndiyo dawa ya kutokuwa na machafuko ya “kikabila”, mbona Somalia, Rwanda na Burundi zimekumbwa na migogoro mikubwa ya kisiasa huku watu katika kila moja ya nchi hizo wanaongea lugha moja tu, yaani, Kisomali, Kinyarwanda na Kirundi! Vilevile, mnamo mwaka 1994 wakati wa mauaji ya kimbari huko Rwanda, *Radio-Television Libre de Milles Collines* ilikuwa ikichochea mauaji hayo kwa kutumia lugha ya taifa, yaani Kinyarwanda!

Sababu ya pili ni kwa serikali kutaka kufuatilia habari zinazochapishwa katika magazeti na kutangazwa kwenye redio. Kwanza, hii ni sababu yenye mtazamo hasi. Serikali inafikiri kuwa watu watatumia lugha zao kwenye vyombo vya habari kufanya mambo yasiyokuwa na manufaa kwa taifa. Msimamo mzuri zaidi ungekuwa kuamini kuwa lugha hizi zitatumika kwa mambo yasiyokuwa na madhara yoyote kwa taifa; yaani kuwapasha habari na kuwaelimisha watu katika jamii husika. Pili, bila shaka serikali ina uwezo wa kufuatilia mambo yanayoandikwa au kutangazwa kwa kutumia lugha za asili kwa sababu katika serikali kuna watu wanaojua lugha hizo au inaweza kuwatumia watu wengine wenye kujua lugha hizo. Haiyumkiniki kuwa jambo linaweza kuandikwa kwa lugha yoyote ya asili na serikali isiwe na uwezo wa kulifanyia utafiti. Jambo la kushangaza ni kuwa msimamo huu wa serikali unapingana na Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 (uk. 17–18) ambayo pamoja na mambo mengine, inasema:

- Jamii zetu zitaendelea kutumia na kujivunia lugha zake za asili.
- Wananchi, mashirika ya umma na ya watu binafsi yatahamasishwa kuandika, kukusanya, kutafiti, kuhifadhi na kutafsiri lugha za asili katika lugha nyingine.
- Uandishi wa kamusi na vitabu vya sarufi za lugha za asili utahimizwa.
- Mashirika ya umma na ya watu binafsi yatahimizwa kuchapisha na kusambaza maandiko katika lugha za asili.

Kwa hakika, lugha ya Kiswahili inatoa msongo mkubwa kwa lugha nyingine za Tanzania na kasi yake haina mfano hapa Tanzania, na pengine hata katika bara zima la Afrika. Hata hivyo, nguvu ya msongo wa Kiswahili kwa lugha nyingine imejengwa kwa makusudi kwa kutumia sera, sheria na kanuni mbalimbali. Hoja ni kwamba kwa kufanya hivyo jamii za wazungumzaji wa lugha nyingine zinanyimwa fursa ya kukuza, kuendeleza na kuhifadhi sehemu muhimu ya utamaduni wao; kwamba taifa zima linatupilia mbali rasilimali kabla ya wakati wake na hivyo kudhoofisha jitihada zetu za kujitea maendeleo; na kwamba taifa linajiweka katika hali ya unyonge kwa kudharau na kupuuza utamaduni wake na hivyo kushindwa kujipambanua vilivyo katika jamii pana ya wanadamu.

#### **Changamoto katika Kukuza Lugha za Asili**

Kuna misimamo mitatu ya kifalsafa kuhusu lugha.

##### *(a) Lugha kama tatizo*

Wenye msimamo huu huona lugha nyingi kama tatizo. Msimamo huu una mizizi yake katika nchi za Ulaya wakati nchi hizo zilipokuwa zinajitahidi kuwa na dola huru. Waliamini kuwa ili nchi/dola iweze kuimarika, lazima kuwe na lugha moja. Hivyo kaulimbiu yao ilikuwa *dola moja, lugha moja*. Iliaminika kuwa lugha nyingine nje ya lugha ya taifa/dola zitavuruga ujenzi wa taifa/dola imara. Msimamo huo ndio tuliourithi kutoka kwa wakoloni, na kwa kiasi kikubwa unaweza kueleza kwa nini serikali ya Tanzania inapinga matumizi ya lugha za asili katika vyombo vya habari na nyanja nyingine rasmi.

##### *(b) Lugha kama haki ya kila mtu*

Msimamo huu unajikita katika imani kuwa kila binadamu anayo haki ya msingi ya kutumia lugha yake ya kwanza katika nyanja zote. Kwa mujibu wa mtazamo huu, kumkataza mtu au kundi la watu kutumia lugha yao ni kuwakosesha haki ya msingi. Msimamo huu vilevile huhusishwa na imani katika uanuai wa lugha. Baadhi ya wanazuoni wamefananisha uanuai wa lugha na bustani yenye maua ya aina nyingi na rangi nyingi, ambayo hakika hupendeza zaidi kuliko ile yenye aina na rangi moja tu ya ua, hata lingekuwa zuri namna gani.

(c) *Lugha kama rasilimali*

Msimamo huu huamini kuwa lugha ni rasilimali kama rasilimali nyingine yoyote. Kwa mtazamo huu taifa likiwa na lugha nyingi, haziwi tatizo bali rasilimali inayoweza kutumika kwa manufaa ya jamii husika. Kama tulivyosema hapo awali, faida ya rasilimali-lugha ni pamoja na kusheheni maarifa ambayo yakitumiwa vizuri yanaweza kuwa chachu ya maendeleo ya taifa.

Tunadhani misimamo mizuri ni kuona lugha kama *haki* na kama *rasilimali*. Changamoto tuliyo nayo ni kuhamasisha jamii zetu na viongozi wetu watambue kuwa lugha za asili sio *tatizo*, na kuwa zinaweza kutumiwa vizuri, kuleta ustawi na maendeleo katika taifa letu. Katika kufanikisha hili, Kahigi (2008) amependekeza mambo yafuatayo yafanyike:

- Kuanzisha vyama vya wataalamu wa lugha za asili pamoja na wakereketwa wa lugha hizo ambao watakuwa mstari wa mbele kuzitetea na kuzikuza kwa kufanya utafiti na kuandika maandiko mbalimbali katika lugha hizo.
- Kutozinyima fursa lugha za asili kutumika madarasani kama lugha za kueleza mambo ambayo wanafunzi hawakuelewa. Hili hasa linaweza kufaa kwa madarasa ya mwanzo huko vijijini ambako watoto huanza shule bila kujua Kiswahili.
- Kuunganisha baadhi ya lugha zinazokaribiana kinasaba ili iwe rahisi kuandika vitabu vinavyoweza kusomwa na watu wengi zaidi.

Kwa teknolojia ya kisasa inawezekana kabisa kuwa na redio yenye kulenga hadhira ya kijiji kimoja, au gazeti lenye wasomaji katika kata moja, au televisheni yenye watazamaji katika wilaya moja. Lakini pia vyombo hivyo vya habari vyaweza kuwa na vipindi mbalimbali kuwalenga wazungumzaji wa lugha mbalimbali katika maeneo makubwa zaidi – kama redio za mataifa mengine zifanyavyo zinaporusha matangazo kwa lugha mbalimbali za dunia.

Fursa ya mtu kuwasiliana na watu wengine kwa lugha aitakayo mtu ni haki ya binadamu. Kutambuliwa kwa haki hii kwa vitendo kutamwezesha mtu mmoja mmoja na jamii moja moja kupata taarifa za mambo yenye kuathiri maisha yake; kutamwezesha kutoa mchango wake katika kujadili kwa uelewa sera na sheria zinazotumika kumtawala; kutamwezesha kuelimika ipasavyo katika kupambana na makali ya maisha. Waelimishaji afya wanaweza kuwafikia watu wengi zaidi katika kampeni za kupambana na maradhi kama ukimwi na malaria. Wanasiasa wanaweza kufafanua sera zao kwa watu na kupata ushiriki mkubwa zaidi hasa kutoka vijijini. Wafanyabiashara wanaweza kutangaza bidhaa zao katika lugha mbalimbali na kuongeza mauzo.

Mfano mmoja wa mchango wa lugha za Tanzania katika kukuza uchumi unatoka katika sekta ya elimu. Fursa ya kujifunza/kufundisha lugha za Tanzania katika ngazi mbalimbali za mfumo wa elimu itatoa ajira kwa walimu

na waandishi wa vitabu vya lugha hizo. Wahitimu wa masomo haya watatengeneza ajira katika kufungua nyanja mpya za mawasiliano – redio, televisheni, magazeti, vipeperushi, tafsiri (za sera, sheria, maandishi mbalimbali ya maarifa). Wananchi wenye uelewa mpana watashiriki zaidi katika kujiletea maendeleo na kujenga taifa lenye watu makini.

Kuthamini lugha zetu kutatupa msukumo mkubwa katika kujiletea maendeleo, kujenga demokrasia, na kuhifadhi utamaduni wetu. Badala ya kutugawa katika makabila kama baadhi yetu tunavyohofu, lugha zetu zitakuwa nyenzo kubwa za kukuza utu wetu kwa hali na mali. Kwa jumla, hofu ya ukabila ni itikadi ya kawaida ya tabaka lo lote la watawala lenye kulenga kuwadhhibiti watawaliwa kwa kisingizio cha kujenga umoja.

## 2. MAANDIKO KATIKA/KUHUSU LUGHA ZA TANZANIA

### Utangulizi

Madhumuni ya sehemu hii ni kuangalia maandiko yaliyopo kuhusu/katika lugha za asili za Tanzania (isipokuwa Kiswahili) ili kujua kazi iliyokwishafanyika kuhusiana na kuchunguza na kurekodi lugha za asili, na pia kubainisha changamoto zinazowakabili watu wenye nia ya kuhifadhi au kukuza lugha hizi.

Mengi ya maandiko yaliyopo yanaweza kukutwa katika bibliografia mbalimbali, mathalani Maho na Sands (2002) na Kagaya na Yoneda (2006), na katika vitabu na majarida yaliyochapishwa baada ya bibliografia hizo kutoka. Kwa kiasi kikubwa, maandiko yaliyopo mengi si ya wasemaji wa lugha hizi, na pia hayakuandikwa kwa lugha za asili. Maandiko haya yanaweza kugawanywa katika makundi mawili:

#### 1. Maandiko ya kitaalamu kuhusu lugha za asili:

- i. tafiti za kilinganishi, kiainishaji na za kiisimu-jamii;
- ii. sarufi (sarufi kamili – yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki), au sarufi vipande, yaani sarufi ya kiwango kimoja au makala juu ya kipengele kimoja; na
- iii. kamusi au misamiati.

Maandiko haya hasa yaliwalenga wataalamu wa lugha, wamisionari na wanafunzi wageni, na mengi yayo yako katika lugha za kigeni. Ingawaje, watafiti hawa walizinufaisha lugha walizozitafiti kwa maandiko yaliyohifadhi sehemu za sarufi na msamiati wake. Baada ya uhuru, utafiti wa namna hii uliendelea, sio tu kwa lengo la kuhifadhi bali pia katika utumizi wa nadharia za kisasa za isimu kutafiti miundo ya lugha za asili.

#### 2. Maandiko katika lugha za asili. Haya yanajumuisha:

- i. vitabu vya kidini (biblia, sehemu za biblia, katekismu, vitabu vya sala na nyimbo, n.k.);
- ii. vitabu vichache vya tafsiri za hadithi na semi (methali na vitendawili) kwa Kiswahili au lugha za kigeni kutoka kwenye lugha za asili; na
- iii. vitabu vichache vya hadithi, semi, historia na tanzu nyingine katika lugha za asili.

Baadhi ya maandiko haya (hasa ya kidini, hadithi, semi na historia) yaliwalenga wasemaji wa lugha hizi, ingawa mengine (yaliyochapishwa katika majarida ya kitaalamu) yaliwalenga wataalamu na wanafunzi wageni wa lugha hizi. Hata hivyo, maandiko mengi ya namna hii hayakuchapishwa kwa sababu hapakuwepo wachapishaji waliokuwa na ujasiri wa kuchapisha vitabu vya lugha za asili. Mfano wa mwandishi ambaye alikosa mchapishaji wa kazi zake za kihistoria, ngano na semi ni Kitereza (1980), mwandishi wa riwaya maarufu ya Bwana

Myombekere na Bibi Bugonoka. Mfano wa mwandishi wa vitabu vya historia aliyefaulu kupata mchapishaji ni Lwamugira (1949).

### Maandiko Yanayohusu Lugha za Asili

*Maandiko ya tafiti za kilinganishi, kiainishaji na kiisimujamii*

Maandiko ya tafiti za kilinganishi na kiainishaji ni kama yale ya Bleek (1862/69), Meinhof (1906, 1910), Johnston (1919/22), Guthrie (1948, 1967/71), Nurse 1979; Maho (1999), Schoenbrun (1997), Heine na Nurse (2000), na Nurse na Phillipson (2003). Umuhimu wa maandiko ya namna hii ni kwamba yanatoa picha ya kijumla kuhusu mahusiano ya kinasaba baina ya lugha hizi, licha ya kutoa mwanga kuhusiana na muundo wake.

Hali ya kiisimujamii imetafitiwa na kurekodiwa katika maandiko mengi mbalimbali, mathalani Polomé na Hill (1980), Bromber na Smieja (2004), Batibo (2005); mengine yanayotokana na juhudi za SIL (tazama Mwita (2008)); na mengine yaliyoko katika vitabu na majarida mbalimbali yanayoendelea kuchapishwa. Mojawapo ya mambo yanayofanywa na maandiko haya ni kutoa picha kuhusu uhusiano baina ya lugha na jamii, na hasa hali ya usemwaji wa lugha hizi, lugha na elimu, sera za lugha na mipango-lugha na athari za mipango-lugha iliyopo kwa lugha nyingi za asili.

Licha ya kutoa mchango mkubwa kwenye taaluma ya lugha za Afrika, maandiko yote yaliyotajwa yanawalenga wataalamu na wanafunzi wa isimu ya lugha za Afrika; hayawalengi wasemaji wa lugha zenyewe.

### Sarufi

Mapitio ya bibliografia yanaonyesha kuwa si lugha zote zimepata kuandikiwa sarufi au hata makala ya kisarufi. Lugha nyingi hazijatafitiwa. Maandiko ya kisarufi yaliyoorodheshwa katika Maho na Sands (2002) na Kagaya na Yoneda (2006) yanaonyesha kuwa ni lugha kama 50 tu kati ya lugha zote za Tanzania ambazo zimeandikiwa angalau sarufi au sarufi “kipande”; aidha, ni lugha kama 36 tu ambazo zimechambuliwa kwa undani na utafiti kuchapishwa katika makala, hasa za kifonolojia. Uchambuzi wa kimofolojia na sintaksia uko nyuma zaidi, kwani ni lugha 18 tu ambazo zimeshachambuliwa (katika vitabu au makala) kisintaksia au kimofolojia. Zaidi ya hayo, karibu maandiko yote hayo yameandikwa kwa lugha za kigeni. Sarufi pekee iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ni ile ya Kihehe iliyoandikwa na Egidio Crema (1987).

### Kamusi na Misamiati

Maandiko ambayo ni mengi zaidi ni misamiati. Ni misamiati ya lugha 87 tu iliyoorodheshwa katika Maho na Sands (2002). Hata baina ya lugha hizi kuna kutofautiana; zipo lugha zenye mikusanyo mingi ya misamiati, mathalani Kiyao (mikusanyo 9) na zile zenye mkusanyo mmoja (kwa mfano Burunge) au miwili (kwa mfano Kijita).

Lugha ambazo zimeorodheshwa kuwa zina kamusi ni 32. Ni wazi kuwa kazi bado ni kubwa.

### Maandiko katika Lugha za Asili

#### *Vitabu vya kidini*

Kwa lugha nyingi za Tanzania, maandiko pekee ambayo yameandikwa kwa lugha hizo ni ya kidini. Kabla lugha za asili hazijaachwa kutumiwa kama lugha za kidini, maandiko haya yalikuwa yakisomwa, na watu wengi vijijini walijua kusoma, na hata kuandika katika lugha zao. Kwa taarifa tulizo nazo (Mojola 1999; Fabian 2008), lugha kama 8 zina biblia kamili, 17 zina agano jipya, na 11 zina sehemu za biblia. Jambo ambalo halifahamiki vizuri ni lugha ngapi ambazo zina katekismu, vitabu vya sala na vya nyimbo.

#### *Hadithi na semi*

Kwa kiasi kikubwa, fasihi-simulizi katika lugha zetu bado ni ya kusimulia tu. Ni kiasi kidogo tu cha fasihi hii kinachoweza kukutwa katika maandiko ya lugha zenyewe. Maandiko haya ni kama vile majarida, vitabu, na tasnifu. Katika machapisho haya kunapatikana hadithi au semi ambazo zimekusanywa au kuchambuliwa, zikiwa na tafsiri kwa lugha lengwa (Kiswahili au lugha ya kigeni). Mifano ya Kihaya (Mulokozi 1986; Mwombeki na Kamanzi 1999) na Kisumbwa (Capus 1897) na mingine kama hiyo, inaonyesha hali hii.

#### *Maandiko mengineyo*

Kabla ya uhuru kulikuwa na magazeti ambayo yalichapisha maandiko ya aina ya makala, hadithi, semi, mashairi, na habari za matukio mbalimbali katika baadhi ya lugha za asili, mathalani *Rumuli*, *Engoma ya Buhaya*, *Ija Webonere*, *Bukya na Gandi* (katika Kihaya); *Lipuli* (Kihehe) na *Lumuli* (Kisukuma). Baada ya uhuru, sera ya kupendelea Kiswahili iliyaua magazeti haya. Siku hizi ni gazeti moja tu, *Rumuli*, ambalo bado lipo; lakini kwa kufuata sera iliyopo, linachapishwa kwa Kiswahili, na andiko moja tu fupi katika Kihaya.

### Changamoto

Mapitio haya mafupi yanadhihirisha changamoto zifuatazo:

1. Ni dhahiri kuwa maandiko mengi yamewalenga wanaisimu, au wanafunzi wa sarufi, na yameandikwa kwa lugha za kigeni (Kiingereza, Kijerumani, Kifaransa, Kireno, n.k.). *Changamoto iliyopo ni namna ya kuwalenga wasemaji wa lugha za asili.*
2. Kwa lugha nyingi sana, sarufi na kamusi (vifaa viwili muhimu katika kujifunza au kuelewa juu ya lugha) haziwezi kuwasaidia wasemaji wa lugha husika kwa sababu vimeandikwa kwa lugha za kigeni. *Changamoto iliyopo ni kuandika sarufi na kamusi zinazoweza kutumiwa na wasemaji wa lugha za asili.*
3. Mojawapo ya matakwa ya lugha kukua katika zama hizi ni kwa wasemaji kuweza kuandika maandiko mbalimbali kwa lugha yao, kwa ajili ya wasomaji

wasemaji lugha hiyo. Kutokana na sera iliyopo, kwa jumla hakuna waandishi wala wasomaji wa namna hii. *Changamoto iliyopo ni kuweza kupata waandishi na wasomaji katika lugha zetu za asili.*

### Maandiko katika Kuhifadhi, Kukuza na Kudumisha Lugha za Asili

Changamoto hizo hapo juu zinaibua masuala ya kuhifadhi na kukuza lugha za asili.

#### *Kuhifadhi*

Maandiko yanaweza kutumika kuhifadhi lugha katika hali mbalimbali. Mfano mzuri wa dhima hii ya maandiko ni Kigiriki cha kale na Kilatini, lugha ambazo hazisemwi tena lakini zimehifadhiwa katika maandiko ya namna mbalimbali na tanzu mbalimbali. Kwa kuwa lugha hizi zimehifadhiwa kikamilifu, zinaweza kufundishwa vyaoni na “kusemwa” na wanavyuo wanaozisoma. Uhifadhi wa maandiko siku hizi umeendelea zaidi kuliko ulivyokuwa zamani. Siku hizi maandiko yanaweza kuhifadhiwa katika nakala ngumu na nakala tepe. Aidha, inawezekana kabisa kuhifadhi maandiko pamoja na usomaji wake kwa sauti. Maana yake ni kwamba sarufi na fasihi ya lugha mahususi vinaweza kuhifadhiwa kama vinavyosemwa bila matatizo.

Kuhusu jukumu hili, juhudi pekee za kuhifadhi lugha hizi ni za watafiti mbalimbali kama vile wanaisimu, watendaji wa mashirika ya kidini, na wanataaluma wengine. Juhudi za watafiti hawa pamoja na changamoto zilizojitokeza ndizo zimezaa Mradi wa Lugha za Tanzania. Lengo la wadau wa mradi ni kuhakikisha kuwa lugha zote zinatafitiwa na kuandikiwa kamusi, sarufi na maandiko ya kifasihi-simulizi. Ni wazi kwamba kunahitajika mkakati wa kitaifa ili kutekeleza nia ya kuhifadhi lugha za asili inayotajwa katika Sera ya Utamaduni.

#### *Kukuza na kudumisha*

Kukuza lugha maana yake ni kuiwezesha lugha hiyo si tu kuendelea kusemwa, kuandikwa na kusomwa na wasemaji wake, bali pia kupanuka katika matumizi na idadi ya wasemaji wake.

Ukuaji huu hauwezi kutokea iwapo:

- i. hakuna sera zinazoruhusu utumizi wa lugha hizi katika miktadha mbalimbali iliyo bayana;
- ii. hakuna motisha (za hali na mali) zinazowasukuma watu wajifunze, waseme, waandike, wasome na kuona fahari kuzitumia lugha hizi katika miktadha hiyo; na
- iii. hakuna mipango madhubuti ya kufundisha lugha hizi katika ngazi zote za elimu.

Lugha inayokua huwa na wasemaji wanaoweza kuiandika, kuisoma, kuisema, kuifundisha na kuirithisha kwa watoto wao. Kwa mantiki hii ukuzaji wa lugha za asili unakabiliwa na changamoto kubwa.

### 3. UAINISHAJI WA LUGHA ZA TANZANIA KINASABA

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi pekee katika bara la Afrika ambamo mbari kuu nne za lugha za Kiafrika zinapatikana. Mbari ya kwanza ni ile ya Naija-Kongo ambayo lugha zake zilizo nyingi ni zile za Kibantu, k.m. Kisukuma, Kinyamwezi, Kiha, Kigogo, Kihaya n.k. Mbari ya pili ni ile ya lugha za Kinilo, kwa mfano, Kiluo na Kimaasai. Mbari ya tatu ni ya Kikushi ambayo inawakilishwa na lugha za Kiiraku, Kiburunge na Kima. Mbari ya mwisho ni ya Kikoisani ambayo inazo lugha kama Kisandawe na Kihadzabe. Wazungumzaji wa lugha za mbari hizi wamefika nyakati tofauti kuishi katika sehemu hii ambayo baadaye imekuja kujulikana kama Tanzania.

Kwa mujibu wa wazungumzaji wa lugha hizo, imeonekana kuwa lugha hizo zinatofautiana sana kwa ukubwa. Kuna lugha zenye wazungumzaji zaidi ya milioni tano, k.m. Kisukuma; kuna zenye ukubwa wa wastani kama wazungumzaji milioni moja lakini hawafiki milioni tano, k.m. Kihaya, Kimakonde na Kigogo; kuna lugha ndogo zenye wazungumzaji wasiotimia laki moja, ambazo ndizo nyingi; na zile ndogo sana zenye wazungumzaji wasiotimia elfu moja. Kwa ujumla mbari hizi nne ndizo zimekuwa chanzo cha kuifanya Tanzania iwe na takribani lugha zisizopungua 150 (Rugemalira na Muzale 2008). Zaidi ya asilimia 85 ya lugha hizi ni za Kibantu na asilimia 15 zilizobaki ni zile zinazowakilisha mbari za Kiniloti, Kikushi na Kikoisani.

Ingawaje idadi ya lugha husika ni nyingi, lakini ukweli uliodhihirika ni kwamba lugha zilizo nyingi, hususani zile za Kibantu zinashabihiana sana kimsamiati na kisarufi. Wachunguzi kadhaa wameainisha lugha za Tanzania (Guthrie 1948, 1970–71; Greenberg 1963; Nurse 1979; Raymond 2005). Kwa kuzingatia tafiti hizi, lugha za Tanzania zimeainishwa kama inavyoonyeshwa katika orodha ifuatayo.

#### Uainishaji Kinasaba wa Lugha za Kibantu za Tanzania

##### I. Ukanda wa Ziwa

###### A. Nyanza Mashariki

1. Mara-Mori (Kikurya, Kingoreme, Kisweta, Kihacha, Kisimbiti, Kikine, Kirieri, Kisurwa, Kikabhwa, Kikiroobha, Kikenye, Kigusii, Kikironi)
2. Serengeti Chini (Kiikizu, Kishashi, Kizanaki)
3. Serengeti Juu (Kinata, Kiikoma, Kiisenye)
4. Suguti (Kijita, Kikwaya, Kiruuri, Kileki)

###### B. Nyanza Magharibi

1. Rutara (Kinyambo, Kihaya, Kisubi, Kizinza, Kilongo, Kikerewe, Kinyankore, Kikiga)
2. Nyanda za Juu Magharibi (Kishubi, Kihangaza, Kiha, Kirundi, Kinyarwanda)
3. Kiganda

##### II. Tanzania Magharibi

- ###### A. Unyamwezi (Kisukuma, Kinyamwezi, Kisumbwa, Kikimbu, Kibungu)

- ###### B. Bonde la Ufa (Kinilamba, Kinyisanzu, Kinyaturu)
- ###### C. Kirangi (Kirangi, Kimbugwe).

### III. Ruvu-Pwani

#### A. Ruvu Kuu

1. Ruvu Magharibi (Kinyambwa, Kigogo, Kikagulu, Kividunda, Kitiliko)
2. Ruvu Mashariki (Kiluguru, Kikutu, Kikami, Kidoe, Kizalamo, Kikwere)
3. Seuta (Kisambaa, Kibondei, Kizigula, Kisagara, Kinguu)

#### B. Pwani

1. Pare (Kiasu, Kitaveta)
2. Sabaki (Kidigo, Kisegeju, Kiswahili, Kipokomo)

### IV. Kilimanjaro

#### A. Kilimanjaro

1. Kilimanjaro Magharibi (Kimashami, Kimeru, Kiwoso)
2. Kilimanjaro Kati (Kimochi, Kiuru, Kikahe)
3. Kilimanjaro Mashariki (Kiroombo, Kivunjo)
4. Kikamba, Kikikuyu

#### B. Ugweno (Kigweno)

### V. Nyasa-Tanganyika

- #### A. Mwika (Kisafwa, Kipimbwe, Kifipa, Kimambwe, Kinyiha, Kinyamwanga, Kibembe, Kitongwe, Kibende)

- #### B. Unyakyusa (Kinyakyusa, Kindali, Kilungu, Kilambya, Kimalila, Kiwanda, Kisongwe, Kiwemba)

### VI. Nyanda za Juu Kusini

- #### A. Ubena (Kibena, Kisangu, Kihehe)

- #### B. Kusini Magharibi (Kiwani, Kikinga, Kikisi, Kipangwa)

### VII. Rufiji-Ruvuma

#### A. Rufiji

1. Kinyasa
2. Kindendeule, Kingindo, Kimatengo, Kinindi
3. Kingoni, Kimanda, Kimpoto, Kindengereko, Kinyagatwa, Kirwingo, Kinkamanga

- #### B. Kilombero (Kipogoro, Kisagara, Kindamba, Kimatumbi, Kindwewe, Kimbunga)

- #### C. Ruvuma (Kiyao, Kimwera, Kimakonde, Kimaraba, Kilomwe, Kimatambwe, Kindonde, Kimakua)

### Uainishaji Kinasaba wa Lugha Zilizokatika Makundi Mengine

- #### A. Lugha za Kikushi: Kialagwa, Kiburunge, Kigorwaa, Kiiraku, Kima, Kisomali

- #### B. Lugha za Kinilo: Kimaasai (Kikwavi, Kimaasai, Kiarusha, Kindorobo); Kidatooga; Kiluo

- #### C. Lugha za Kikoisani: Kihadzabe, Kisandawe

### Lugha ambazo hazijaainishwa

- #### Kilingala (Kigoma), Kibwali (Kigoma), Kisonjo (Arusha)

## 4. ISTILAHU

Katika sehemu hii tutatoa ufafanuzi wa istilahi mbalimbali utakaomsaidia msomaji kuelewa vizuri atlas hii. Istilahi husika zinaeleza uhusiano kati ya lugha na jamii, au baina ya lugha na lugha.

### *Lugha na Lahaja*

Kwa maelezo mafupi tunaweza kusema *lugha* ni mfumo wa maneno yaliyoundwa na jamii fulani ya watu, kwa kutumia sauti au alama za nasibu (ambazo si lazima ziakisi maana), kwa madhumuni ya kuwasiliana katika maisha na shughuli zao za kila siku. Katika atlas hii ya Lugha za Tanzania kuna jumla ya lugha 150 ambazo zimeonyeshwa.

Kwa kiasi kikubwa hadi hii leo wataalamu hawajakubaliana juu ya nini kiitwe *lugha* na nini kiitwe *lahaja*. Kwa mtazamo wa jumla, *lahaja* ni namna nyingine ya usemaji wa *lugha* ileile moja. Ingawa kuna tofauti za wazi kati ya wasemaji wa lahaja tofauti, hali hiyo haiwazui kuelewana. Kwa mfano, baadhi ya lahaja za lugha ya Kisukuma ni Kidakama, Kinyantuzu, King'weli. Vilevile baadhi ya lahaja za Kihaya ni Kiziba, Kinyaihangiro, Kihyoza, na Kihamba. Na baadhi ya lahaja za Kimaasai ni Kipurko, Kilumbwa (Kikwavi), na Kisongo.

Hata hivyo, wazungumzaji wa lahaja mbili za lugha moja wanaweza kudai kwamba wanazungumza lugha tofauti kwa kuzingatia mambo mengine ya kijamii, kama vile maeneo ya makazi, historia, idadi ya wasemaji, na mipaka ya utawala. Mfano mzuri ni wasemaji wa lugha za *Kiruuri*, *Kijita* na *Kikwaaya*. Utafiti wa Massamba (1977) umeonyesha kuwa katika mtazamo wa kiisimu lugha hizo tatu zinaweza kuhesabika kuwa lahaja tatu za lugha hiyohiyo moja, kwani kila msemaji wa lugha hizi humwelewa mwenzake kwa urahisi kabisa tukiacha tofauti ndogondogo zilizopo. Lakini kwa upande wa wazungumzaji wenyewe, kila mmoja wao anajihesabu kuwa anazungumza “lugha” tofauti na wala si lahaja.

### *Lugha na Kabila*

Kihistoria kumekuwapo uhusiano wa karibu kati ya lugha na jina la jamii au kabila lenye lugha hiyo. Kwa mfano, Wahehe wanazungumza Kihehe; Wahacha wanasema Kihacha; Wakwere wanasema Kikwere. Hata hivyo, si lazima kuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya lugha na kabila. Kwa mfano, watoto wengi wanaozaliwa sehemu za mijini hawaongei lugha za wazazi wao; lugha yao ni Kiswahili ingawa makabila yao ni tofauti. Mfano mwingine unahusisha jamii (kabila) ya Wapare ambao hujipambanua katika lugha mbili, yaani Kigweno na Kiasu, na hakuna lugha ya “Kipare”.

Mfano wa tatu unahitaji maelezo zaidi, nao unahusisha matumizi ya neno “Kichagga” katika atlas hii ya lugha za Tanzania. Jamii ya Wachagga ina asili yake katika mkoa wa Kilimanjaro, na lugha sita za jamii hii zimetambuliwa, yaani Kimochi, Kimashami, Kirombo, Kivunjo, Kiuru na Kiwoso. Lakini Wachagga waliopatikana katika mikoa mingine, hawakubainishwa wanazungumza lugha ipi kati ya hizo sita. Kwa hivyo Wachagga hao, mahali popote Tanzania nje ya mkoa wa Kilimanjaro, wamehesabiwa kuwa wanasema lugha ya “Kichagga”.

### *Lugha ya Kwanza na Lugha ya Pili*

*Lugha ya kwanza* ni lugha ambayo mtu hujifunza anapoanza kusema; yaani lugha ambayo mtu hujifunza kutoka kwa wazazi au walezi wake kutoka utotoni. Pengine huitwa ‘lugha ya mama’, ingawa inawezekana mtoto akajifunza lugha ya watu wengine ambao sio mama wala baba, kwa kutegemea mazingira anayolelewa. *Lugha ya Pili* ni lugha yoyote ambayo mtu hujifunza baada ya kuwa tayari ana lugha yake ya kwanza. Mara nyingi mtu hujifunza lugha ya pili ukubwani, baada ya kuondoka katika mazingira ya nyumbani na kukutana na jamii zenye kuzungumza lugha nyingine. Watu walio wengi pia hufundishwa lugha ya pili shuleni.

Katika atlas hii takwimu zinaonyesha wazungumzaji wa lugha husika ambao kwao ni lugha ya kwanza, bila kujali kama watu hao wamejifunza lugha nyingine yoyote kama lugha ya pili. Katika kila kijiji au mtaa kila mkazi anabainishwa kuwa ni msemaji wa lugha moja tu ya kwanza. Iwapo kuna lugha zaidi ya moja katika eneo husika, basi lugha moja yenye wasemaji wengi (kama lugha yao ya kwanza) kuliko nyingine inaonyeshwa katika ramani kama lugha kuu ya kwanza. Lugha inayofuata kwa wingi wa wasemaji (kama lugha yao ya kwanza) katika eneo hilo inaonyeshwa kama lugha kuu ya pili. Na lugha ya tatu kwa idadi ya wasemaji (kama lugha yao ya kwanza) inaonyeshwa katika ramani kama lugha kuu ya tatu, n.k. hadi ngazi tano. Kwa maana hii, atlas hii inaonyesha kwamba wasemaji wa lugha ya Kisukuma kama lugha yao ya kwanza ni wengi kuliko wasemaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Vivyo hivyo wasemaji wa Kigogo kama lugha ya kwanza ni wengi kuliko wasemaji wa Kihaya kama lugha ya kwanza.

### *Jina Dhalilishi la Lugha*

*Jina dhalilishi* la lugha ni jina la kuitaja lugha kwa kuibeza lugha hiyo na jamii ya wazungumzaji wa lugha hiyo. Majina hayo kwa kawaida hutungwa na majirani au maadui wa jamii husika. Baadhi ya majina dhalilishi ni Kimang’ati, Kitaturu, na Kikonongo.

## 5. MAUDHUI YA ATLASI NA MBINU ZA UTAFITI

Atlasi ya lugha za Tanzania ni kiungo muhimu katika mkakati huu wa kuzitambua na kuzithamini rasilimali hizi za utamaduni. Inatupa picha ya hali halisi kwa taifa zima kuhusiana na mambo yafuatayo:

- i) kuna lugha zipi na ziko wapi;
- ii) kila lugha ina wazungumzaji wangapi;
- iii) lugha gani ina wazungumzaji wengi kuliko zote; ipi ni ndogo kuliko zote;
- iv) lugha zipi ziko katika hatari kubwa zaidi ya kutokomea;
- v) maandiko yapi yako katika lugha hizi;
- vi) lugha zimesambaa kiasi gani katika mikoa na wilaya kadhaa;
- vii) lugha zipi zina maelewano ya karibu.

Taarifa zinazopatikana katika atlasi hii zimetokana na utafiti wa miaka kadhaa. Kiini cha taarifa hizi ni takwimu za idadi ya wazungumzaji wa kila lugha. Namna moja nzuri ya kupata takwimu za aina hii ni kuhesabu wazungumzaji wa kila lugha kutoka nyumba hadi nyumba kama ifanyikavyo katika sensa ya idadi ya watu kitaifa. Ingetazamiwa kuwa katika sensa ya taifa ya idadi ya watu, baadhi ya maswali yangelenga kutafuta taarifa kuhusu lugha. Lakini kwa kuwa ilishindikana kuingiza maswali ya lugha katika sensa ya mwaka 2002, mradi ulilazimika kubuni njia mbadala ya kupata taarifa hizi. Kwa kutumia data za sensa ya mwaka 2002 watoa taarifa walikadiria kwa kila kijiji au mtaa, idadi ya wazungumzaji wa kila lugha katika kijiji hicho. Makadirio haya yalilenga lugha mama tu (yaani lugha ya kwanza ya mzungumzaji) na siyo lugha nyingine ambayo mtu amejifunza ukubwani au shuleni. Hata hivyo, zilitambuliwa lugha kuu zisizozidi tano kwa kila kijiji. Maeneo yenye lugha zaidi ya tano kwa mtaa mmoja yalipatikana katika miji na majiji, hususani Dar es Salaam na Mwanza (wilaya ya Nyamagana). Hivyo hakuna takwimu za maeneo hayo katika atlasi hii na utaratibu wa pekee unahitajika kuyashughulikia.

Taarifa nyingine zinajumuisha matokeo ya utafiti wa wataalamu mbalimbali kama zinavyopatikana katika machapisho kadhaa yanayoorodheshwa katika marejeo. Taarifa hizo, kwa mfano, zinahusu uainishaji wa lugha kinasaba, lahaja za lugha, majina mbadala ya lugha, na maandiko katika lugha za Tanzania.

### Utengenezaji wa Ramani za Atlasi

Taarifa za watafiti wa lugha zilikusanywa na kupangwa kwa kata kwenye programu ya kompyuta ya *Ms Excel*, zikionyesha lugha kuu ya 1, ya 2 ya 3 n.k. Programu ya *MapInfo Professional* ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia, imetumika kuunganisha taarifa za watafiti wa lugha na ramani za kata zilizotengenezwa na Taasisi ya Taifa ya Takwimu za mwaka 2002. Ramani zinazoonyesha kusambaa kwa lugha zimezalishwa kwa kutumia rangi mbalimbali.

Kwa kila mkoa na wilaya, ramani zinazoonyesha lugha

kuu ya **kwanza**, ya **pili** na ya **tatu** zimewekwa kwa mfuatano ili msomaji aweze kuona uhusiano wa lugha kuu tatu kwa kila mkoa na wilaya. Takwimu za idadi ya watu wanaoongea lugha husika pia zimeonyeshwa kwenye ufunguo wa kila ramani. Taarifa za barabara, mito na majina ya kata zimeonyeshwa kwenye ramani ili kumsaidia mtumiaji kupata mwelekeo. Katika kusoma kila ramani, msomaji anashauriwa kufungua ramani inayoonyesha lugha ya pili na ya tatu ili kuuona uhusiano uliopo kati ya lugha mbalimbali.

Msomaji anatahadharishwa ya kuwa upana wa maeneo yanayoonyesha rangi kuwakilisha lugha sio wingi wa watu wanaozungumza lugha hiyo. Sehemu nyingine, lugha inaonekana kuchukua eneo kubwa kwa vile hata kata za sehemu hizo ni kubwa, au kwa vile sehemu hizo ni hifadhi ya misitu au mbuga za wanyama.

### Atlasi kwenye Nakala Tepe

Atlasi hii inapatikana pia kwa nakala tepe katika sidii.

## 6. ORODHA YA VITABU VYA MRADI

	Mwandishi	Jina la Kitabu	Mchapishaji	Mwaka
<b>Kamusi</b>				
1	J. Rugemalira	<i>Msamiati wa Runyambo–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2002
2	H. Muzale	<i>Kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2004
3	D. Massamba	<i>Kamusi ya Ciruuri–Kiswahili -Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2005
4	C. Rubagumya	<i>Msamiati wa Kihangaza–Kiswahili -Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2006
5	H. Muzale	<i>Kamusi ya Kihaya –Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2006
6	J. Rugemalira	<i>Kamusi ya Kimashami–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
7	Y. Rubanza	<i>Msamiati wa Luzinza–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
8	A. Mreta	<i>Msamiati wa Kisimbiti–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
9	S. Sewangi	<i>Msamiati wa Kiikizo–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
10	J. Mdee	<i>Msamiati wa Kijita–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
11	K. Kahigi	<i>Kamusi ya Kisumbwa–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
12	A. Mreta	<i>Kamusi ya Chasu–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
13	Y. Rubanza	<i>Msamiati wa Kimeru–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
14	S. Sewangi	<i>Msamiati wa Kigweni–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
15	G. Mrikaria	<i>Msamiati wa Kimochi–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
16	K. Kahigi	<i>Msamiati wa Kikahe–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
17	J. Kiango	<i>Msamiati wa Kibondei–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
18	Z. Mochiwa	<i>Msamiati wa Kizigula–Kiswahili-Kiingereza</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
<b>Sarufi</b>				
19	J. Rugemalira	<i>A Grammar of Runyambo</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2005
<b>Juzuu za Makala Mbalimbali</b>				
20	Mradi	<i>Occasional Papers in Linguistics 1</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2005
21	Mradi	<i>Occasional Papers in Linguistics 2</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
22	Mradi	<i>Occasional Papers in Linguistics 3</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2008
<b>Hadithi za Jadi</b>				
23	K. Legere & P. Mkwana'hembo	<i>Hadithi za Kividunda</i>	TUKI	2006
24	K. Legere & P. Mkwana'hembo	<i>Hadithi za Zamani za Kividunda</i>	Benedictine Publications, Ndanda	2008
<b>Atlasi</b>				
25	Mradi wa Lugha za Tanzania	<i>Atlasi ya Lugha za Tanzania</i>	Mradi wa Lugha za Tanzania	2009

**Marejeo**

- Batibo, H. 2005. *Language Endangerment and Death in Africa: Causes, Consequences and Challenges*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Bleek, Wilhelm H.I. 1862/69 *A Comparative Grammar of South African Languages*. Cape Town & London: J.C. Juta & Trubner & Co.
- Bromber, K. na B. Smieja (Wahariri) 2004. *Globalization and African Languages: Risks and Benefits*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Capus, A. 1897. Contes, Chants, et Proverbes des Basumbwa dans l'Afrique Orientale. *Zeitschrift fuer Afrikanische und Oceanische Sprachen*, 3: 358–381.
- Crema, Egidio. 1987. *Sarufi ya Lugha ya Kihehe*. Irole: Tanzania. (Amechapisha mwenyewe).
- Fabian, D.N. 2008. Nafasi ya Tafsiri za Biblia katika Kukuza Lugha Tanzania. Katika: *Occasional Papers in Linguistics* No. 2. Mradi wa Lugha za Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. uk. 62–73.
